# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# WIZARA YA AFYA

## MKATABA MDOGO WA LOCAL FUNDI UJENZI WA NYUMBA YA MTUMISHI

## KATIKA

## HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA WA SONGWE

**NOVEMBA, 2021**

# MKATABA WA UJENZI

## MKATABA WA KUJENGA NYUMBA YA MTUMISHI

Mkataba huu umefungwa kati ya Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Songwe **S.L.P. 301, Songwe** (ambaye katika mkataba huu atajulikana kama mwajiri) kwa upande mmoja

**NA**

**WAZIRI MOHAMED WANGARA S.L.P 545 SONGWE** ambaye katika mkataba huu atajulikana kama Fundi Mkuu (Local fundi) kwa ajili ya **KUJENGA NYUMBA YA MTUMISHI**

Fundi mkuu (Local fundi) atafanya kazi ya kujenga **NYUMBA YA MTUMISHI** kwa thamani ya shilingi **Milioni Kumi na Nane na Laki Tano Tu (TSHS. 18,500,000.00).**

**1.0 TAFASIRI**

Makubaliano haya yamefanyika na kushuhudiwa kama ifuatavyo:-

**1.1** Fundi mkuu (Local Fundi) maana yake ni mtu aliyeingia mkataba na Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Songwe kwa ajili ya **kujenga Nyumba ya Mtumishi.**

1.2 Hospitali maana yake ni Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Songwe.

**2.0 Utoaji wa huduma hii**

Fundi mkuu/ Local fundi atafanya kazi ya kujenga nyumba ya mtumishi.

2.1 Pale patakapokuwa na hitaji maalumu kutoka Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Songwe na sio vinginevyo.

2.2 Fundi mkuu/Local fundi atatakiwa kufanya kazi hiyo ndani ya muda wa **miezi miwili na siku 10 kuanzia tarehe 05 Aprili,2022 hadi tarehe 15 Juni. 2022.**

2.3 IwapoFundi mkuu/Local fundi atachelewa kuanza na kumaliza kazi hiyo kama inavyotakiwa katika mkataba huu, mwajiri atakuwa na mamlaka ya kuvunja mkataba huu na kuajiri Fundi mkuu/Local fundi mwingine.

2.4 Mkataba huu utasomeka pamoja na nyarala zifuatazo:

- Barua ya Tunzo
- Barua ya kukubali Tunzo
- Schedule of labour
- Michoro
- Muhtasari wa majadiliano

**3.0 MALIPO.**

3.1Mkandarasi/Fundi atalipwa kwa hatua zifuatazokadri anavyoendelea na ujenzi na baada ya mwajiri kukagua na kuridhika na jengo husika.

A. Ujenzi wa kuta za msingi.
B. Zege la jamvi, Nguzo za awali na Mkanda wa chini (Ground beam).
C. Ujenzi wa Boma na nguzo
D. Ring beams, linterna kuta baada ya ring beams.
E. Kuezeka / Kupaua.

F. Plasta na Floor screed
G. Ngazi na Ngazi mtelezo.
H. Mifumo ya awali ya maji safi na maji taka (ndani ya jengo) na mifumo ya awali ya umeme.
I. Marumaru za kuta na sakafu
J. Brandering na kufunga gypsum boards
K. Skimming na Rangi.
L. Wayaring ya umeme na mfumo wa zima moto
M. Mfumo wa maji safi na maji taka (nje ya jengo) na ujenzi wa mashimo ya vyoo.
N. Usafi kuzunguka jengo na kuondoa mabaki ya vifaa.

3.2 Malipo yatakuwa kwa hundi/Benki baada ya Fundi mkuu/ Local Fundi kuwasilisha madai na kwa kuzingatia aya ya 3.1 ya mkataba huu.

3.3 Fedha ya zuio (Retention money) itakua asilimia 5 (5%) ya malipo na itakatwa kuanzia hati ya malipo namba mbili na italipwa baada ya kipindi cha matazamio ya uharibifu kukamilika.

## 4.0 MUDA WA MKATABA NA TATHIMINI YA MKATABA.

4.1 Mkataba huu ni wa kipindi cha Miezi miwili na siku 10 tu.

4.2. Mkataba unaweza kufanyiwa tathimini na mapitio kwa niaba ya Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Songwe ili kujiridhisha na kiwango na ubora wa utendaji kazi wa Fundi mkuu/Local fundi.

4.3 kipindi cha matazamio ya uharibifu (Defect liability period) kitakua miezi sita (6) tangu fundi mkuu kukabidhi kazi.

## 5.0 WAJIBU WA FUNDI MKUU/LOCAL FUNDI

5.1 Fundi mkuu/Local fundi anatakiwa kufanya kazi kama alivyoagizwa na Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Songwe na kwa muda muafaka na katika ubora unaotakiwa.

5.2 Fundi mkuu/Local fundi hatoruhusiwa kutoa kazi hii kwa mtu mwingine au chombo chochote kingine bila kibali cha mwajiri (Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Songwe).

5.3 Fundi mkuu/Local fundi atawajibika kwa uharibifu wowote utakaosababishwa na uzembe wa watumishi wake au yeye mwenyewe wakati wa utekelezaji wa mkataba na hata baada ya kumalizika kwa mkataba.

## 6.0 WAJIBU WA MWAJIRI

6.1 Mwajiri atawajibika kuweka mazingira bora ya kumuwezesha Fundi mkuu/Local Fundi kufanya kazi yake kwa ufanisi.

6.2 Mwajiri atawajibika kumletea fundi vifaa vya ujenzi katika eneo la ujenzi kwa muda Muafaka.

## 7.0 MUDA WA MAKUBALIANO

7.1 Mkataba huu ni wa kipindi cha miezi minne tangu Fundi mkuu kukabidhiwa eneo la ujenzi na baada ya hapo mkataba mwingine unaweza kuwekwa kwa makubaliano ya pande zote mbili.

7.2 Pamoja na maelezo yaliyopo hapo juu, iwapo kutakuwepo na uvunjaji wa mkataba,

matangazo yatatolewa kumpata Fundi mkuu/Local fundi mwingine kwa ajili ya kufanyakazi hata kabla ya kumalizika kwa muda wa mkataba huu.

7.3 Sheria zitakazotumika katika mkataba huu ni sheria za Tanzania.

7.4 Iwapo itatokea mgogoro kati ya pande zinazounda mkataba huu, njia ya mazungumzo itatumika na ikishindikana atatafutwa msuluhishi atakayekubalika na pande zote mbili.

7.5 Pande zote mbili zitaingia makubaliano haya kwa hiari, akili timamu bila kulazimishwa wala kushurutishwa.

Mkataba huu unaingiwa na kutiwa saini leo hii tarehe ……05 APRILI……mwaka 2021.

**KWA NIABA YA HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA WA SONGWE**

JINA: ……Dr. J. LULANDALA……
SAHIHI ……[signature]……

CHEO: MKURUGENZI MTENDAJI HOSPITALI YA RUFAA MKOA WA SONGWE

TAREHE: ……11/04/2022……

**MHURI WA OFISI**

SHAHIDI WA MWAJIRI
JINA: ……RAPHAEL ERNEST MUELLA……
SAHIHI ……[signature]……
CHEO……AFISA UGAVI……
TAREHE ……05/04/2022……

**KWA NIABA YA FUNDI MKUU/LOCAL FUNDI**
JINA: ……WAZIRI MOHAMED WANGARA……
SAHIHI ……[signature]……
CHEO ……FUNDI UJENZI……
TAREHE ……05/04/2022……

SHAHIDI WA FUNDI MKUU/LOCAL FUNDI
JINA: ……SAMWELI RICHARD MAYALLIGA……
SAHIHI ……[signature]……
CHEO ……MFANYABIASHARA……
TAREHE ……05/04/2022……

**MBELE YA MWANASHERIA**

JINA: ……J. SILOMBA……
SAHIHI ……[signature]……
CHEO ……WAKILI……
TAREHE……11/4/2022……